

# MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Barua Pepe: [gcla@gcla.go.tz](mailto:gcla@gcla.go.tz)  
Simu Nambari: 255 – 22 – 2113383/4  
Nukushi: 255 – 22 – 2113320.

05 BARABARA YASECHERELA,  
S.L.P. 2925  
DODOMA.



## TAARIFA KWA UMMA

### KUSITISHWA KWA MATUMIZI YA MFUMO WA USIMAMIZI WA WATEJA WA KEMIKALI TOLEO LA KWANZA (CCMP I)

Dodoma, 10 Januari, 2025

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inawataarifu wadau wote wa kemikali nchini na watumiaji wa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Mteja wa Kemikali Toleo la Kwanza (Customer Chemicals Management Portal I - CCMP I) juu ya kusitishwa kwa matumizi ya Mfumo huo **kuanzia tarehe 19 Januari, 2025 Saa Sita kamili (6:00) usiku.**

Matumizi ya Mfumo huo Toleo la Kwanza (CCMP I) yanasitishwa baada ya kukamilika na kuundwa kwa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Mteja wa Kemikali Toleo la Pili (CCMP II) ambao unatokana na maboresho ya Toleo la Kwanza pamoja na kuendana na maboresho yaliyofanyika kwenye mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mabadiliko hayo ya usitishwaji wa matumizi ya *CCMP I* kwenda *CCMP II* hayatarajii kuleta athari yoyote kwa Mteja/Mdau wa Kemikali kwa kuwa, taarifa zote za wateja zitahamishwa moja kwa moja kutoka *CCMP I* kwenda *CCMP II* kwa kuzingatia hali halisi zinavyoonekana kwenye toleo la kwanza.

Baada ya kusitishwa kwa Mfumo wa *CCMP I* kwa tarehe iliyoitajwa, wateja/wadau wote waliosajiliwa wataendelea kupata huduma kama kawaida kupitia mfumo wa *CCMP II*. Mamlaka inaomba radhi kwa wateja/wadau kwa usumbufu wowote utakaojitokeza kutokana na kusitishwa kwa mfumo tajwa hapo juu.

Kwa maswali na msaada zaidi, tafadhali tembelea Ofisi za Mamlaka zilizopo karibu yako, au piga simu namba: **0737878021**, **0737878027** na **0737878028** zote zinapatikana pia kwa njia ya WhatsApp, au barua pepe [support@gcla.go.tz](mailto:support@gcla.go.tz).

Imetolewa na;

Sylvester S. Omary

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO NA UHUSIANO KWA UMMA**